

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

**HOTUBA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU AZIMIO LA
KURIDHIA UBADILISHAJI HADHI MAPORI YA AKIBA YA BIHARAMULO,
BURIGI, KIMISI, IBANDA NA RUMANYIKA-ORUGUNDU KUWA HIFADHI
ZA TAIFA**

(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge la Toleo la
Januari, 2016)

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
DODOMA

Februari, 2019.

HOTUBA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA UBADILISHAJI HADHI MAPORI YA AKIBA YA BIHARAMULO, BURIGI, KIMISI, IBANDA NA RUMANYIKA-ORUGUNDU KUWA HIFADHI ZA TAIFA

(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge la Toleo la Januari, 2016)

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema na Upendo kwa kiniweka hai na mwenye nguvu na kjuweza kusimama hapa mbele ya hadhira hii ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya AZIMIO lililo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kufikisha kwa wataanzani wote salama za Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Mheshimiwa Esther Matiko ambao wako Magereza Segerea kwa usemi unaosema kwamba; “ **Patriotism is loyalty to the country ALWAYS, Loyalty to the Government when it deserves it**”

Mheshimiwa Spika, kwa nukuu hiyo tafsiri isiyo rasmi “**Uzalendo ni Utii kwa nchi yako wakati wote na Utii kwa Serikali pale inapostahili**” Kambi Rasmi ya Upinzani ina wajibu wa Kikatiba wa kuhoji matendo ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Tutakuwa watiifu pale tu

Serikali inapostahili na inapotimiza majukumu yake na kutupa sababu ya kuipenda nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kwa muktadha huo ni wajibu wetu kuhakikisha Serikali haifanyi jambo lolote ambalo litariharibu taifa letu. Tukumbuke kwamba Serikali huja na kuondoka lakini nchi liko pale pale.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ni miongoni mwa nchi zilizobahatika kuwa na vivutio vingi vya utalii katika ukanda wa Afrika hivyo kuwa ni nchi yenye fursa kubwa inayoweza kutumia sekta hii ya utalii katika kuinua uchumi wake. Sekta ya Utalii ndiyo sekta inayoingiza fedha nyingi za kigeni na pia inauwezo wa kutoa ajira nyingi za moja kwa moja na zile ambazo sio ajira za moja kwa moja kama vile kupitia kwa kile kinachoitwa **multiplier effect** kwenye ajira zitokanazo na utalii.

Mheshimiwa Spika, katika hoja iliyo mbele yetu ya Serikali kuliomba Bunge kuridhia kupandishwa hadhi kwa mapori ya akiba kuwa hifadhi za Taifa, ikiwa na lengo la kupanua maeneo ambayo yatakuwa yanasimamiwa na TANAPA na hivyo kuongeza maeneo ya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha Tanzania inaeneo la kilometa za mraba 945,234. Kati ya eneo hilo takriban robo ya eneo hilo(236,308.8 sq.km) imeachwa kwa ajili ya matumizi ya wanyama pori. (Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba). Usimamizi wa maeneo ya wanyamapori unahusisha hifadhi za taifa 16 zinazosimamiwa na TANAPA, Mapori ya akiba 28, na Mapori tengefu 42 ambayo yanasimamiwa na TAWA.

Mheshimiwa Spika, Mapori ya akiba yanayotakiwa kupandishwa hadhi ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika-Orugundu ni miongoni mwa mapori yanayosimamiwa na TAWA. Mapori hayo yanajumla ya kilometa za mraba 5251, ambapo mapori matatu ya Burigi, Biharamulo na Kimisi yanazungukwa na kata 18 zenye vijiji 48. Aidha, Mapori ya Ibanda na Rumanyika yanazungukwa na Kata 12 zenye vijiji 24. Kwa ujumla ni kuwa eneo ambalo linapandishwa hadi lina jumla ya kata 30 na vijiji 72.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa maeneo haya ni maeneo ya wafugaji wengi sana, hivyo basi ni ukweli kuwa maeneo haya mara nyingi ynakuwa na mgogoro baina yao na Serikali katika kutafuta maeneo ya malisho kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, Upandishwaji wa hadi wa mapori sio jambo la kutoa kauli tu au kuletwa kwa sheria Bungeni na kuipitisha, bali ni jambo linaloendana na uwekezaji wa kutosha katika maeneo husika ili maeneo hayo yawe na hadhi ya kuwavutia watu kutembelea maeneo hayo. Uwekezaji katika maeneo husika ni miundombinu kama barabara, mawasiliano ya uhakika na mahotel kwenye maeneo husika na pia na kuwa na aina mbalimbali ya bidhaa za kiutalii ambazo zitaweza kuwekwa sokono ili kuwavutia watalii

2. MAUDHUI YA AZIMIO

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema kuwa uridhiwaji wa azimio hili, ni kuwa Taifa litapata manufaa yafuatayo;

- i. Kuimarisha uhifadhi wa maliasili hususan wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine wa kwenye maji; na
- ii. Kuongeza pato la Taifa kwa msingi kuwa ubadilishaji hadhi wa mapori hayo ya akiba kutasababisha hifadhi hizo kuwa vivutio vya Utalii.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ni kweli lakini kwa kuwa maeneo husika yanayopandishwa hadhi yapo chini ya TAWA na hivyo uhifadhi bado upo pale pale, hivyo kupandishwa kwa hadhi kwa maeneo hayo kuwa hifadhi badala ya mapori ya akiba ni kuongeza matumizi kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuongeza pato la taifa, sio jambo la kutoa kauli bali pato linaongezeka kutokana na uwekezaji utakaofanyika katika eneo husika. Ili kupata fedha inabidi utumie fedha, hivyo tuna mashaka makubwa kama kweli azma iliyokusudiwa itafikiwa au itakuwa ni mzigo tu kwa hifadhi zingine.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Tanapa zinaonesha kuwa kati ya hifadhi 16 zilizo chini yake ni hifadhi 5 tu ndizo zinajiendesha kwa faida na hivyo kuweza kuziendesha hifadhi zingine 11 zilizobakia. Hii inatokana na ukweli kwamba uwekezaji unaofanywa kwenye hifadhi zetu hauzifanyi hifadhi zetu kuwa shindani na hifadhi za jirani zetu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja za msingi ambazo tungependa tupatiwe majibu na Serikali, kwamba miaka yote Serikali imekuwa ikijitahidi kujenga miundombinu ili kuufanya ukanda wa kusini na nyanda za juu kusini kuwa kituo cha utalii na ndio mojawapo ya sababu ya kuhakikisha uwanja wa ndege wa Iringa na Songwe

uvilivyojengwa na kukarabatiwa ingawa bado havijafikiwa kiwango kinachotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Magufuli wakati wa Sherehe ya Mei Mosi mwaka 2018 mkoani Iringa alisema Serikali imelenga kuimarisha utalii Kanda ya Kusini. Aliongeza na kusema kuwa wananchi walizoea kufanya utalii maeneo ya Kaskazini wakati Ruaha ni mbuga kubwa yenye vivutio bora lakini haikutembelewa na watalii kwa kuwa miundombinu haijaboreshwa. Ni kwanini tuache ambapo tayari kuna fahamika na kuanza kuwekeza sehemu ambayo haitahitaji nguvu nyingi sana ya uwekezaji hadi kuanza uzalishaji?

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba ukanda wa kusini ndio uliokuwa katika mipango ya Serikali kuufanya kuwa kituo kingine cha utalii baada ya Ukanda wa Kaskazini (Tourist destination), sasa hii haraka inayoletwa hapa kupandisha mapori hayo ya akiba kuwa hifadhi kwa minajili ya kuufanya ukanda wa ziwa MAGHARIBI kuwa kivutio cha Utalii wakati ukweli ni kwamba uwekezaji bado ni mdogo kulinganisha na uwekezaji ambao tayari umefanyika kwa ukanda wa kusini haraka hiyo inatoka wapi? Kambi Rasmi ya Upinzani tunaona hii sawa na kufukuza sungura wawili kwa wakati mmoja jambo ambalo linaweza kupelekea kukosa sungura wote wawili. Kuna msemu usemao “ **You cannot chase to Rabbits at the same time**”

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaonyesha kumekuwa na mtafaruku wa matumizi ya maeneo husika baina ya wafugaji na wakulima kwa miaka kadhaa ambapo wananchi wengi wamepoteza mifugo yao na wengine wako magerezani kwa kushindwa kulipa faini. Serikali zote za

CCM zilizopita zilikwishaliona tatizo hilo na zilikuwa katika mchakato wa kuachia baadhi ya mapori kati ya hayo yanayopandishwa hadhi kuwa ni kwa matumizi ya wananchi. Je, mchakato huo umefikia wapi? **Mheshimiwa Spika**, imetulazimu kuhoji jambo hilo kutokana na ukweli kwamba kata 30 na vijiji 72 vinavyozunguka eneo husika na ukweli kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa wakati ambapo ardhi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu inabaki kuwa ni ileile, hili ni jambo la hatari sana kwa wanayamapori kupewa umuhimu mkubwa kuliko wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari maandalizi yameisha kamilika ili kutimiza azma ya Serikali ya kuyapandisha hadhi mapori hayo tajwa, tunaomba wataanzania wajulishwe, je wananchi wanaozunguka mapori husika wanapangiwa mkakati gani ili waweze kuendesha maisha yao ya kila siku bila ya uwepo wa uvunjifu wa amani na ukiukwaji wa haki zao za msingi kama ambavyo imetokea pale mifugo yao na wao wenyewe walivyodhalilishwa katika operesheni kadhaa zilizoendeshwa na Serikali?

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, tunafahamu umuhimu wa uhifadhi katika nchi yetu, kama ambavyo tumejaribu kueleza hapo awali, lakini ni jambo la msingi kuwa badala ya kufanya uhifadhi wa wanyapori na bioanuwai ni vyema pia tukahakikisha kuwa wananchi nao wanakuwa na amani katika mioyo yao ili waweze kushiriki katika uhifadhi huo na uhifadhi uwe na maana kwao.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba hadi sasa kuna mikopo imeshatolewa na taasisi za kimataifa ili kuhakikisha **Southern circuit** inakuwa ni kitovu kingine cha utalii sambamba na kile cha kaskazini. Lakini tumeshindwa kuona mkakati huo kama unatekelezeka kwa vitendo zaidi ya kuwa kwenye makaratasi tu. Je tatizo nini? Na kwa taarifa tulizonazo Kambi ya Upinzani World Bank wanasita kutoa pesa kwa ajili ya kuimarisha utalii Kusini (Regrow) kwa kile kinachodaiwa Serikali kukiuka makubaliano ya awali.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyohoji hapo awali kuhusu baadhi ya mapori kati ya hayo yanayopandishwa hadhi kukabidhiwa kwa wananchi ili yatumike kwa shughuli zao za kiuchumi kwa minajili ya kuondoa migongano baina ya Serikali na wananchi hao ambao sehemu kubwa ni wafugaji, suala hilo liliishia wapi?

Mheshimiwa Spika, kauli ya majuzi ya Mheshimiwa Rais kuhusu kuwaacha wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi kama walikuwa wanafanya shughuli zao za kutafuta riziki kuendelea kufanya hivyo na wasisumbuliwe, je jambo hili kwa njia moja ama nyingine si linakinzana na kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

.....

Peter Simon Msigwa, Mb

WAZIRI KIVULI-WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

9/2/2019